

SEKTA YA KILIMO

UTANGULIZI

Mkoa wa Njombe una hali nzuri ya hewa ambayo imegawanyika katika nyanda kuu tatu ambazo zinaweza kustawisha mazao mbalimbali kama ifuatavyo:-

- i) **Ukanda wa chini:** Ukanda huu hulimwa mazao ya Mhogo, Mpunga, Karanga, viazi vitamu, korosho, Mtama, mbogamboga, matunda ya ukanda wa joto na migomba.
- ii) **Ukanda wa kati:** Mazao yanayostawi katika Ukanda wa Kati ni Mahindi, Maua, Maharage, Alizeti, Njegere, Migomba, Ngano, Viazi mviringo, Mbogamboga, Chai, Kahawa, Pareto na Matunda.
- iii) **Ukanda wa Juu:** Ukanda huu hulima mazao makuu ya Chakula ya Mahindi, Maharage, Viazi mviringo, ngano, njegere, alizeti, mbogamboga na matunda ya ukanda wa baridi, kwa Mazao ya biashara ni Chai, Kahawa, Pareto na Ngano.

Mkoa wa Njombe una ukubwa eneo la kilomita za mraba **24,994**. Eneo linalofaa kwa kilimo ni hekta. **1,090,000** na kati ya hiyo eneo lililolimwa kwa msimu 2017/18 ni hekta **374,637** sawa asilimia **34%** ya eneo linalofaa kwa kilimo.

MAZAO YA CHAKULA

Mkoa wa Njombe una mazao makuu wawili (2) kwa ajili ya chakula yaani mahindi na viazi mviringo ambapo wakati mwingine mazao hayo hutumika kwa biashara pia, hasa yanapozalishwa kwa kiwango cha ziada. Mazao haya huzalishwa katika kila Halmashauri ndani ya Mkoa wa njombe, ambapo tangu mwaka 2013 – 2019 uzalishaji wa mahindi ni kati ya 38% - 42% na Viazi mviringo ni kati ya 40% - 47% ya mazao ya chakula. Mazao ya chakula yanayozalishwa katika Mkoa yapo katika makundi matatu yaani mazao ya nafaka (Mahindi, mpunga, mtama, ulezi, uwele na ngano), mazao ya mizizi (Viazi mviringo, viazi vitamu na mihogo) na mazao ya jamii ya mikunde (maharage, kunde, njegere, njugu na maharage ya soya).

Uzalishaji wa mazao ya mahindi na Viazi mviringo umeoneshwa katika jedwali Na. 1 & 2

Jedwali Na. 1 Uzalishaji wa mahindi

Halmashauri	2013/14		2014/15		2015/16		2016/17		2017/18		2018/19	
	Hekta	Tani	Hekta	Tani	Hekta	Tani	Hekta	Tani	Hekta	Tani	Hekta	Tani
Njombe Mji	25,226	113,513	25,208	113,436	25,287	114,018	25,451	113,728	25,471.36	114,637.82	24,576	103,592
Njombe DC	55,490	138,725	57,176	171,528	58,320	174,960	59,486	178,458	60,676	182,028	62,507	187,521
Ludewa DC	46,447	100,882	45,120	97,999	45,220	97,520	53,130	111,500	45,000	94,500	43,788	91,955
Wanging'ombe DC	47,310	199,863	47,309	199,863.1	44,450.50	104,446.20	44,513.60	114,274	47,463.50	128,151.45	49,836.15	91,157.04
Makambako TC	12,478	31,195	11,850	26,662.50	15,246	36590.4	10,403.0	26,319.6	12,605.45	31,513.63	9,320	20,503.32
Makete DC	15,103	30,206	15,106	30,212	14,516	29,032	13,851.00	29,695.50	14,996.00	32,481.34	15,347	32,228.70
Jumla	202,054	614,384	201,769	639,701	203,040	556,567	206,835	573,975	206,212	583,312	205,374	526,957

Jedwali Na. 2 Uzalishaji wa Viazi Mviringo

Halmashauri	2012/13		2013/14		2014/15		2015/16		2016/17		2017/18		2018/19	
	Hekta	Tani	Hekta	Tani	Hekta	Tani	Hekta	Tani	Hekta	Tani	Hekta	Tani	Hekta	Tani
Njombe Mji	18,471	155,198	18,806	324,403	14,116	243,504	18,502	166,889	18,590	303,427	18,604.9	353,027.9	19,023	367,200
Njombe DC	16,431	248,955	841	12,615	840	12,600	892	13,380	910	13,650	928	13,926	954	14,310
Ludewa DC	2,402.5	1,988.7	2,190	1,200	4,636	35,357	4,636	10,750	3,600	28,800	3,750	30,000	2,844	22,752
Wanging'ombe DC	0	0	16,433	247,195	12,641.60	193,224.84	9,990.05	47,106	12,409.7	138,865	16,316.2	176,244.96	17,132	185,335.7
Makambako TC	1,500	22,500	901.64	11,920.90	408	4,896	383	4596	128.4	1,781.0	288	3,456	204.2	1,021
Makete DC	12,715	127,150	10,234	102,340	12,757	118,370	11,470	57,455	11,690	128,557.8	11,991	119,913	12,899.8	167,697
Jumla	51,520	555,792	49,406	699,674	45,399	607,952	45,873	300,176	47,328	615,080	51,878	696,568	53,057	758,316

MAZAO YA BIASHARA.

Mazao ya biashara yanayozalishwa katika mkoa wa Njombe ni Chai, Alizeti, Kahawa, karanga, Korosho, Pareto na matunda hasa parachichi. Mazao haya hustawi vizuri kutokana na hali ya hewa ya maeneo husika kama ilivyooneshwa katika jedwali Na. 3

Jedwali Na. 3 Uzalishaji wa mazao makuu ya biashara kwa kila Halmashauri

Halmashauri	Aina ya zao
Njombe TC	Parachichi na Chai
Njombe DC	Chai, Kahawa, Parachichi na alizeti
Ludewa DC	Kahawa, Alizeti, korosho, Karanga, Pareto
Wanging'ombe DC	Alizeti, Parachichi, karanga, Kahawa, Pareto
Makambako TC	Alizeti, Parachichi
Makete DC	Matofaa(Apples), Parachichi, Karanga, Pareto

Aidha uzalishaji wa mazao hayo kimkoa kuanzia msimu wa kilimo 2013/14 hadi 2017/18 umeoneshwa katika jedwali Na. 4

jedwali Na. 4 Uzalishaji wa mazao ya biashara kimkoa

Zao	2013/14		2014/15		2015/16		2016/17		2017/18	
	Hekta	Tani	Hekta	Tani	Hekta	Tani	Hekta	Tani	Hekta	Tani
Alizeti	17,838	23,510	26,958	9,168	21,802	26,117	15,497	14,743	14,020	28,577
Chai	8,003	39,025	7,987	12,344	35,418	39,177	47,150	52,585	8,149	51,201
Kahawa	243	134	902	108	896	109	924	131	281	107
Pareto	3,388	2,838	1,483	1,781	1,001	790	970	667	1,395	1,095
Koroshoh	794	7.94	757	5	1,053	5	2,091	12	2,100	64
Karanga	7,667	5,091	9,639	13,038	7,690	4,759	4,273	5,161	5,464	6,976
Apple (Matofaa)	345	869	328	1,157	361	1,283	594	1,216	599.82	1,176.82
Chungwa	23	20	26	32	23	54	261	784	36.52	162.76
Embe	165	261	223	3,839	97	59	289	182	1,611.24	1,137.76
Mapeasi (Pear)	476	1,338	489	1,481	576	1,550	489	1,244	417.19	1,257.95
Ndizi	1,374	5,340	1,575	5,914	630	5,954	1,357	3,961	1,452.26	14,860.88
Papai	8	40	18	45	4	12	20	40	761.43	994.14
Plum	305	589	306	812	309	807	338	852	335.83	817.50
Peaches	583	1,467	660	1,582	667	1,351	664	1,345	583.80	1,241.60
Parachichi	843	6,848	1,163	10,567	1,109	4,944	1,494	3,338	2,080.49	6,071.68
Nanasi	420	2,926	424	3,000	448	3,163	473	3,286	476.80	3,286.10
Mapera	66	201	50	108	47	79	46	71	48.50	69.40
Stafeli	36	57	36	57	40	57	41	57	41.00	58.00
Tikitimaji	486	1,024	1,001	4,206	106	742	2,082	14,681	1,902.67	6,834.48
Limao	15	52	15	54	5	12	7	16	7.67	14.33
Jumla	43,078	91,637.94	54,040	69,298	72,282	91,024	79,040	104,332	41,764.22	126,003.4

FURSA ZA UWEKEZAJI KATIKA SEKTA YA KILIMO.

1. Uwekezaji katika uzalishaji wa mbegu bora za viazi mviringo.

Upatikanaji wa mbegu bora za viazi mviringo katika Mkoa wa Njombe ni asilimia 2% - 4% ya mahitaji ya mbegu za viazi. Wakulima wengi wanatumia mbegu za zamani za mwaka 1987 ambayo inaitwa CIP au Kikondo. Mbegu hizo zimepoteza ubora wake ikiwa ni pamoja na kushambuliwa na magonjwa na kuzalisha kiasi kidogo kwa eneo. Uwezo wa kuzalisha kwa mbegu za CIP kwa sasa ni tani tani 5 -7 kwa hekta. Wakati mbegu bora huzaa hadi kufikia tani 25 – 30 kwa hekta. Makisio ya mahitaji ya mbegu bora kwa mkoa wa Njombe ni kama inavyoonekana katika jedwali Na. 5

Jedwali Na. 5 Makisio ya mahitaji ya mbegu bora za viazi mviringo

Halmashauri	Eneo linalolimwa (Hekta)	Kiasi cha mbegu za Viazi Mviringo kwa hekta(Tani)	Jumla ya Mahitaji ya mbegu ya Viazi Mviringo(Tani)
Ludewa DC	3,750	2.5	9,375
Makete DC	11,991.3	2.5	29,978
Njombe TC	18,604.87	2.5	46,512
Wanging'ombe DC	16,316.20	2.5	40,791
Njombe DC	928	2.5	2,320
Makambako TC	288	2.5	720
JUMLA KIMKOA	51,878		129,696

2. Uwekezaji kwenye miundombinu za upimaji wa afya udongo.

Huduma hii kwa sasa haipatikani katika maeneo ya wakulima. Huduma ya afya ya udongo hushughulika na kupima sampuli za udongo kujua uwiano wa virutubisho vilivyoko kwenye udongo ambavyo huhitajika na mimea kwa ajili ya ukuaji na uzalishaji wenye tija. Upimaji wa udongo ni muhimu sana kwa sababu huonesha viwango vya virutubisho vilivyoko kwenye udongo kulingana na aina ya zao linalozalishwa. Pale itakapoonekana hakuna ulinganifu wa virutubisho, ndipo mkulima hulazimika kuongeza aina ya virutubisho vilivyopungua au kukosekana kwa kiwango kinachotakiwa ili mimea iwe na chakula cha kutosha isiyo na madhara.

Zao linalozalishwa likikosa chakula cha kutosha hutoa mazao kidogo ambayo hayatarudisha gharama za uzalishaji, hivyo mkulima hupata hasara na mazao kidogo yatakayovunwa yatakuwa na upungufu wa virutubisho au viini lishe kwa ajili ya afya ya binadamu. Kuonesha umuhimu wa kupima afya udongo, Matokeo ya baadhi ya virutubisho kwenye sampuli za udongo iliyotokana na utafiti uliyofanywa na wadau mbali mbali katika sekta ya kilimo yameoneshwa katika jedwali Na. 6.

Matokeo yanayoonekana kwenye jedwali Na. 6 yanaonesha kuwa sampuli zote 32 za udongo zilizopimwa, hakuna hata mmoja ilikuwa na virutubisho ya kutosha kwa ajili ya uzalishaji wa mazao husika. Aidha hakuna sampuli ambazo matokeo yalifanana. Hii inaonesha kuwa matokeo ya eneo mmoja hayawezi kutumika kupata mahitaji ya mbolea ya eneo lingine. Hivyo kila eneo ni lazima lipimwe peke yake na matokeo yake kutumika kwa eneo hilo tu kupata virutubisho vilivyopungua kwenye udongo. *Eneo la upimaji wa udongo ina fursa kubwa ya uwekezaji kwani kwa sasa huduma hii haipatikani, pamoja na umuhimu wake hasa katika uzalishaji wenye tija na wenye kukidhi virutubisho vinavyohitajika kwa afya binadamu na wanyama.*

Jedwali Na. 6 Viwango vya upungufu wa virutubisho katika udongo katika maeneo yaliyopimwa sampuli za udongo kati ya mwaka 2014 –2017.

Halmashauri	Vijiji	P	K	Ca	Mg	S	Fe	B	Zn	Cu	Mn	Mo	
Ludewa DC	Shaurimoyo S1	92%	7%	56%	0%	90%	0%	47%	73%	68%	0%	53%	
	Shaurimoyo S2	88%	19%	62%	0%	80%	0%	55%	85%	63%	0%	52%	
	Shaurimoyo S3	85%	61%	72%	0%	90%	0%	46%	68%	32%	0%	50%	
	Shaurimoyo S4	88%	7%	76%	0%	90%	0%	40%	73%	32%	0%	47%	
	Amani S1	73%	39%	74%	0%	90%	0%	49%	51%	0%	0%	47%	
	Amani S2	85%	49%	76%	0%	60%	0%	49%	85%	32%	0%	68%	
	Mavanga S1	42%	0%	23%	0%	90%	0%	59%	15%	0%	0%	75%	
	Mavanga S2	23%	0%	18%	0%	90%	0%	53%	39%	0%	0%	67%	
	Mavanga S3	69%	0%	70%	0%	90%	0%	59%	76%	0%	0%	58%	
	Mavanga S4	69%	0%	28%	0%	80%	0%	45%	7%	0%	0%	72%	
	Mbugani	38%	0%	25%	0%	90%	0%	34%	39%	0%	0%	78%	
	Lugarawa	85%	25%	51%	0%	90%	0%	51%	66%	12%	0%	77%	
	Njombe DC	Igongolo S1	77%	33%	70%	0%	90%	0%	49%	68%	68%	0%	0%
		Kaduma	87%	32%	83%	33%	20%	0%	41%	32%	14%	0%	0%
Makambako TC	Ikwete	62%	39%	68%	0%	90%	0%	51%	5%	51%	0%	0%	
	Lyamkena S1	69%	36%	81%	0%	90%	0%	47%	66%	63%	0%	0%	
	Lyamkena S2	69%	36%	81%	0%	90%	0%	47%	66%	63%	0%	0%	
	Lyamkena S3	27%	53%	72%	0%	90%	0%	65%	34%	59%	0%	0%	
	Utengule	89%	0%	53%	0%	60%	59%	41%	73%	43%	0%	71%	
Njombe TC	Utalingolo S1	88%	78%	93%	58%	80%	0%	58%	83%	80%	40%	0%	
	Utalingolo S2	89%	17%	65%	44%	80%	60%	55%	68%	67%	0%	0%	
	Utalingolo S3	83%	85%	90%	76%	0%	55%	59%	83%	62%	0%	0%	
	Yakobi	88%	68%	85%	22%	90%	0%	65%	85%	49%	53%	0%	
	Mgodechi	88%	100%	93%	100%	50%	99%	66%	85%	0%	97%	0%	
	Iwungilo	87%	72%	73%	23%	80%	69%	51%	85%	43%	0%	13%	
Wanging'ombe DC	Igagala	93%	77%	87%	61%	80%	0%	48%	83%	5%	0%	0%	
	Usalule S1	93%	2%	49%	0%	90%	48%	49%	76%	67%	0%	0%	
	Usalule S2	83%	0%	62%	0%	50%	0%	27%	0%	0%	57%	71%	
	Igima	93%	0%	59%	0%	90%	40%	53%	90%	76%	0%	0%	
	Mafinga	93%	77%	78%	7%	90%	54%	49%	80%	52%	0%	0%	
Makete DC	Lupila	93%	18%	76%	12%	90%	42%	66%	73%	76%	0%	0%	
	Isapulano	98%	55%	68%	39%	90%	33%	63%	32%	86%	0%	33%	

3. Uwekezaji katika ujenzi wa maghala na usambazaji wa pembejeo za kilimo hasa maeneo ya vijijini.

Pembejeo nyingi kwa sasa ziko mjini hali inayowafanya wakulima kuchukulia pembejeo mijini kipindi cha msimu wa kilimo. Mkoa wa Njombe una vijiji 386 kati ya vijiji hivyo ni vijiji 90 sawa na 23% ambavyo vina wauzaji wa pembejeo za kilimo. Kwa Mkoa wa njombe kuna vituo viwili ambavyo mbolea hupatikana kwa wingi na kuwa na bei ya jumla na rejareja. Vituo hivyo ni makambako Mjini na Njombe Mjini. Vituo hivyo vina miundombinu ya maghala makubwa ya kuhifadhia mbolea hali inayofanya mbolea nyingi kuhifadhiwa katika vituo hivyo.

Halmashauri ambazo mbolea hazifiki kwa wingi kwa sababu ya kutokuwa na mghala ni Njombe Vijijini, Wanging'ombe, Makete na Ludewa. Mkoa wa Njombe una Halmashauri 6 na kati ya hizo 4 hazina miundombinu ya maghala ya kuhifadhia mbolea. Kutokuwa na miundombinu ya kuhifadhi mbolea inaathiri upatikanaji wa pembejeo katika Halmashauri za Njombe Vijijini, Wanging'ombe, Makete na Ludewa ikiwa ni pamoja na mbolea kutokupatikana kwa wakati kwa wakulima. Hii ni fursa kwa wawekezaji kwani wakulima wengi wako katika Halmashauri hizo NNE. Taarifa iliyooneshwa kwenye jedwali Na. 7 ilikusanywa Januari, 2019 toka Halmashauri zote za Mkoa wa Njombe ambapo **98.6%** za mbolea zilikuwa Makambako Mji na Njombe Mji na kipindi hicho ilikuwa ni ya mahitaji makubwa ya mbolea kwa wakulima.

Jedwali Na. 7 Upatikanaji wa mbolea (tani) kwa Halmashauri za Mkoa wa Njombe.

Halmashauri	Mbolea DAP	Mbolea UREA	Mbolea zingine	Jumla	Asilimia ya mbolea
Ludewa DC	40.80	15.35	34.87	91.02	0.6%
Makambako TC	3,166.58	3,092.70	2,649.99	8,909.27	61.3%
Makete DC	11	8	12.80	31	0.2%
Njombe DC	22.9	3.925	14.05	41	0.3%
Njombe TC	1,889.00	571.1	2,956.40	5,417	37.3%
Wanging'ombe DC	17	18.38	17.01	52	0.4%
Jumla Kuu	5,146.65	3,709.46	5,685.12	14,541.23	100%

4. **Uwekezaji katika usindikaji wa mazao ya mahindi kwa ajili ya unga na alizeti kwa ajili ya mafuta.**

i. Mahindi ya ziada

Uzalishaji wa zao la mahindi kila mwaka unaonesha mahindi huzalishwa kwa kiwango cha ziada ambayo huuzwa ili wakulima wajipatie kipato. Hali hii mara nyingi imewafanya wakulima kutafuta masoko na ikipatikana mahindi hununuliwa kwa bei ambayo haina faida kwa wakulima kwa sababu wakulima huuza mahindi ghafi. Makadirio ya mahindi yanayosindikwa kwa mwaka katika Mkoa ni tani 50,000 sawa na 12%- 14% ya mahindi ya ziada. Hivyo kuna fursa ya kusindika kiasi cha mahindi kilichosalia. Mahindi ya ziada yameoneshwa katika dedwali Na. 8

Jdedwali Na. 8 Mahindi ya ziada.

Halmashauri	2014/15	2015/16	2016/17	2017/18	2018/19
Ludewa DC	75,328	75,335	71,535	61,557	59,011
Makambako TC	11,270	14,330	4,059	8,311	0
Makete DC	2,076	0	0	5,643	8,176
Njombe DC	123,806	154,381	157,879	160,824	166,317
Njombe TC	65,589	66,168	65,788	82,435	71,389
Wanging'ombe DC	147,492	42,319	52,147	88,136	51,142
Jumla	425,561	352,533	351,408	406,906	356,035

ii. Alizeti

Alizeti ni moja ya zao la biashara ambayo ina fursa nyingi ndani ya Mkoa, Nchi na Nje ya Nchi hasa kwa ajili ya mafuta ya kupikia na mashudu kwa ajili ya chakula cha mifugo. Kwa sasa mafuta ya kupikia yanayotumika ndani ya Mkoa wa Njombe, zaidi ya 70% ni alizeti ambayo hutolewa katika mikoa wa Singida na Dodoma. Kwa sasa uzalishaji wa zao hili ni mdogo kutosheleza mahitaji ya mafuta ya kupikia na mahitaji ya wasindikaji wa alizeti ndani ya Mkoa.

jedwali namba 9. Uzalishaji wa zao la alizeti

Halmashauri	2014/15	2015/16	2016/17	2017/18
Ludewa DC	4,276	4,176	2,040	48
Makambako TC	891	728	1,056.3	562
Makete DC	146	979.6	114.7	131.6
Njombe DC	995	963.3	1,014	1,045

Njombe TC	52	51	51.3	0
Wanging'ombe DC	2808	19,219	1,0467	11,502
Jumla	9,168	26,116.9	14,743.3	13,288.6

5. Uwekezaji katika uzalishaji wa zao la Parachichi.

Zao la parachichi ni zao ambalo uhitaji wake unaongeza kwa kiasi kikubwa hasa katika masoko ya nje ya nchi. Kutoka na uwepo wa soko, kumekuwa na hamasa kubwa miongoni mwa wakulima katika kujishughulisha na kilimo cha zao la parachichi. Kwa kuwa mkoa wa njombe una hali nzuri ya hewa ambayo inaruhusu uzalishaji wa zao parachichi hivyo kuna fursa kubwa ya uzalishaji wa zao la parachichi katika Mkoa wa njombe. Kwa kuwa maeneo mengi yapo chini ya umiliki wa wakulima, njia bora ya kufanya uwekezaji huu ni kuingia mikataba na wakulima. Wakulima watazalisha mazao kwa ajili ya mwekezaji ambapo mwekezaji atashirikiana na serikali kuwafundisha wakulima mbinu bora za kuzalisha parachichi zinazokidhi soko alilionalo.

Jedwali Na. 10 Uzalishaji wa parachichi kwa tani

Halmashauri	2014/15	2015/16	2016/17	2017/18
Ludewa DC	1,060	1,360	1,120	1,189
Makambako TC	222	360	450	1,436
Makete DC	70.3	74.9	77.1	69.7
Njombe DC	1,527	1,605	1,699	1,672
Njombe TC	49	39	233.3	512.39
Wanging'ombe DC	7,635	1,506	762	1,188
Jumla	10,563.3	4,944	4,341.4	6,067.09